LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA MKATABA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

# SHERIA YA MKATABA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

SHUKRANI ....................................................................................5
DIBAJI ...........................................................................................5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU...................................................................................7
MAONO ........................................................................................8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI ...........................................8
LENGO KUU ..............................................................................8
Utangulizi .............................................................................9
Mfungwa ni nani? ..............................................................9
Aina za adhabu...................................................................10
Adhabu ya Kifungo Gerezani .......................................11
Utumikiaji wa Kifungo Gerezani...................................11
Msamaha kwa wafungwa ............................................12
Sheria ya Msamaha kwa wafungwa..........................14
Bodi ya kitaifa ya msamaha kwa wafungwa...............15
Bodi ya Mkoa ya Msamaha kwa wafungwa...................15
Akiwa nje kwa msamaha wa bodi; anatimiza masharti yaliyowekwa na bodi hiyo. ...........................................17
Utaratibu wa kupeleka maombi ya msamaha kwenye bodi ...................................................................18
Utaratibu wa kusikiliza maombi ya msamaha kwa wafungwa.....................................................................19
Hitimisho............................................................................20

## SHUKRANI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kutoa shukrani kwa wanasheria wake wote, wakiwemo wale wa kujitolea, walioshiriki katika uandaaji wa kijarida hiki. Pia Kituo kinawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki katika kuandaa toleo hili, hususani mwanasheria Hosea Maina Peter na Winnie Sengo pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inaababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria

au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.**

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam, ofisi ndogo zipo Arusha na Dodoma.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa Sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. Utangulizi

Masuala yanayohusu mikataba nchini yanasimamiwa na Sheria ya Mikataba Sura ya 345 iliyorekebishwa mwaka 2019. Katika msingi wa mahusiano ya wanajamii vipo vitu vingi vinatuunganisha na kutufanya kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuleta maendeleo. Hali hii inayofanya mwanadamu lazima aishi na kuhusiana na wanadamu wengine inaleta dhana na uwepo wa makubaliano mbali mbali kila siku. Kila siku mtu utakuwa kwenye makubaliano fulani na mtu mwengine. Makubaliano hayo yanaweza kuwa ya kazi au nauli unalipa kupata usafiri, au unanunua bidhaa n.k.

Makubaliano haya ndio msingi wa neno mkataba. Mkataba si lazima uwe kwenye maandishi unaweza kuonekana kwa maneno au namna ya vitendo baina ya wahusika.

## 2. Maana Ya Mkataba

Kwa tafsiri ya kawaida mtu anaweza kusema mkataba ni makubaliano baina ya pande mbili au zaidi. Hata hivyo Sheria inayoongoza masuala ya mikataba inaeleza kwamba;

Mkataba ni makubaliano baina ya pande mbili au zaidi yanayofanyika kwa mdomo au maandishi yenye nguvu ya kisheria.

Maana hii ya kisheria inaleta taswira tofauti kabisa baina ya makubaliano ambayo tumezoea kuyafanya kila siku na makubaliano ambayo yapo kwa mujibu wa sheria.

## 3. Misingi ya sheria ya mkataba

Si makubaliano yote ni mkataba. Ili makubaliano yawe mkataba kuna vigezo maalum ambavyo lazima pande husika wavizingatie kabla ya kuingia kwenye makubaliano hayo. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo;

### 3.1. Utashi huru/ridhaa/idhini:

Kwamba pande zinazoingia

makubaliano lazima wayafanye kwa hiyari yao pasipo kushawishiwa au kulazimishwa au kudanganywa kwa namna yoyote ile.

**3.2. Uwezo wa kuingia kwenye mkataba;**

Hapa ili makubaliano yawe na nguvu ya kisheria lazima yawe yameingiwa na pande ambazo zina mamlaka na uwezo wa kisheria kuingia makubaliano. Mfano anayeingia makubaliano ya mkataba lazima awe amefikia umri wa kuanzia miaka 18 na mwenye akili timamu.

**3.3. Utekelezaji halali kisheria**

Yaani malipo yanayotokana na makubaliano lazima yawe halali kisheria, mfano malipo ya mkataba yanaweza kuwa fedha. Si halali kisheria kuwa watu walipane kitu ambacho hakitambuliwi kisheria. Mfano huwezi kuingia mkataba huku malipo yakawa kumpatia upande wa pili mtoto.

### 3.4. Jambo la makubaliano liwe linakubalika kisheria:

Jambo husika ambalo pande zinazoingia mkataba zinakubaliana lazima liwe linakubalika na sheria. Huwezi kuingia mkataba kwa kufanya jambo la kihalifu/kijinai huo ni mkataba haramu. Mfano huwezi kuingia mkataba wa kulipwa kwa kufanya mauwaji ya mtu maana kitendo cha kuua mtu ni jinai kimekatazwa na sheria. Hivyo mkataba kama huo ni batili.

## 4. Uvunjaji wa mkataba na matokeo yake

### Kuvunja mkataba ni nini

Ni ile hali ya kutotekeleza matendo au majukumu yale mliokubaliana ndani ya mkataba husika kwa makusudi, haijalishi mkataba huo ni wa makubaliano ya maandishi

au wa makubaliano ya mazungumzo tu, kama hujatekeleza wajibu wako na majukumu yaliyooanishwa katika mkataba husika kwa makusudi hapo utakuwa umevunja mkataba.

Mfano: mkataba wenu ni wa makubaliano ya maandishi, na unahusisha kuuziana nyumba kwa kiasi cha fulani, ila mlikubaliana mnunuzi akulipe pesa zote ndani ya miez mitatu, kama ikitokea mnunuzi kashindwa kukulipa pesa ndani ya miezi mitatukama masharti yanavyosema kwenye mkataba atakuwa amevunja mkataba. Hiyo ndio maana ya Kuvunja mkataba.

## 5. Jinsi ya kuutekeleza mkataba uliovunjwa

Siku zote, kwenye mkataba husika yule anaekeuka masharti au Kuvunja mkataba ndiye anaestahili kumlipa mwenzake ambaye kwa namna moja au nyingine kaingia kwenye hasara kwa mkataba kuvunjikaa.

Kama sheria ya mikataba Namba 345 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, inavyoelezea katika kifungu cha 73 kifungu kidogo cha Kwanza.Na ikaendelea kusema kwenye kifungu cha 73 kifungu kidogo cha pili cha sheria hiyo hiyo ya mikataba kuwa, hasara ambayo mtu kaipata kutokana na kuvunjikaa kwa mkataba atalipwa iwapo hasara hiyo aliyoipata sio ya siri.

Na kifungu cha 75 cha sheria ya mikataba iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, imeelezea kuwa kimfano mtu ameubatilisha mkataba wa halali kwa makusudi kwa kutotekeleza majukumu ya kimkataba anatakiwa kulipa fidia kwa madhara aliyomsababishia mwenzake.

Na kama mkataba unaelezea kama mmoja wao atavunja mkataba atatakiwa kulipa kiasi kadhaa au kitu chochote kama mkataba unavyoelekeza, basi atatakiwa kulipa kiasi hicho, kama kifungu cha 74 kifungu kidogo

cha nne cha sheria ya mikataba inavyoelezea.

## 6. Vyombo vya utatuzi wa migogoro ya mikataba

Sheria za mikataba zipo nyingi sana hata hivyo iwapo kutajitokeza mgogoro juu ya mikataba vipo vyombo au hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kutatua mgogoro huo;

**6.1. Usuluhishi wa pande za mkataba;**

Hapa pande husika wanajaribu kukaa na kutatua changamoto iliyojitokeza wenyewe

**6.2. Usuluhishi kwa kuhusisha mtu mwengine**

Hapa pande husika zinakubaliana na kuteua mtu wa tatu ambaye hana upande ili kuwasaidia kutatua mgogoro.

**6.3. Kufungua mashitaka kwenye mahakama za madai:**

Endapo pande husika zimeshindwa

kufikia makubaliano wanaweza kufungua madai kwenye mahakama zenye mamlaka.

**6.4. Kupeleka mgogoro kwenye chombo maalum ambacho kilianishwa ndani ya mkataba:**

kuwa endapo mgogoro utajitokeza kitakuwa na mamlaka ya kuamua.

## 7. Muda wa kufungua kesi ya uvunjaji wa mkataba

Muda wa kufungua kesi ya mtu aliyevunja mkataba unaanza palepale mkataba ulipovunjika, na sheria inaelezea uvunjaji wa mkataba mwisho wa kufungua kesi

yake ni miaka 6, ikipita hapo mtu hana mamlaka au uwezo wa kufungua kesi ya uvunjaji wa mkataba.

Ila kuna hali inatokea humfanya mtu kushindwa kufungua kesi mpunakwisha ukakwisha, mtu huyu anaweza kupewa nafasi

na waziri mwenye mamlaka nusu ya muda wa kufungua kesi za uvunjaji wa mikataba, lakin kama anasababu maalumu kama ugonjwa, Kama ilivyoelezea katika kifungu cha 11 kwenye sheria ya kikomo Sura ya 89 ilyorekebishwa 2019.

## 8. Hitimisho

Sheria za mikataba ni moja kati ya sheria ambayo tunaiishi kila siku ingawa hatuitilii maanani. Ni vyema mwananchi akawa makini na makubaliano mbali mbali anayofanya ikiwezekana apate ushauri wa kisheria kabla ya kufanya makubaliano na ahakikishe anafanya makubaliano ya maandishi. Mwananchi anapaswa kutambua ya kwamba si kila makubaliano ni mkataba lakini kila mkataba ni makubaliano.

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

FORD FOUNDATION

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

Ministry for Foreign Affairs of Finland

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV